JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

*Anwani ya Simu*: "ELIMU"
**DAR ES SALAAM**
Simu:+255 22 211-3139, +255 22 211 0146-10
Baruapepe: info@moe.go.tz
Tovuti: www.moe.go.tz
*Unapojibu Tafadhali Taja:*

7 Mtaa wa Magogoni
S. L. P. 9121
**11479 DAR ES SALAAM**

**Kumb. Na**. ED/OKE/NE/Vol. I/01/71

**Tarehe: 25/5/2016**

Makatibu Tawala (M),
Wathibiti Wakuu wa Ubora wa Shule (K),
Katibu Mtendaji (NECTA),
**TANZANIA BARA.**

## WARAKA WA ELIMU NAMBA 3 WA MWAKA 2016 KUHUSU UTEKELEZAJI WA ELIMUMSINGI BILA MALIPO

### 1.0. Utangulizi

Serikali, kupitia Waraka wa Elimu Namba 5 wa Mwaka 2014, imeamua kutoa Elimumsingi (kuanzia Elimu ya Awali hadi Kidato cha Nne) bila malipo. Azma hii ya Serikali ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 ambayo ina lengo la kuhakikisha kwamba watoto wote wa kitanzania wenye rika lengwa la Elimumsingi wanapata elimu bila kikwazo chochote ikiwemo ada au michango.

Katika utekelezaji wa Elimumsingi bila malipo Nyaraka na Miongozo ifuatayo ilitolewa:

i. Waraka wa Elimu Namba 5 wa Mwaka 2015;

ii. Waraka wa Elimu Namba 6 wa Mwaka 2015 kuhusu utekelezaji wa elimu bila malipo;

iii. Mwongozo wa matumizi ya fedha za Ruzuku ya Uendeshaji (Capitation Grant) kwa Shule za Msingi za Serikali Kufuatia Uamuzi wa Serikali Kutekeleza Elimumsingi bila malipo;

iv. Mwongozo wa fomu ya kujiunga na Kidato cha Kwanza katika shule za Sekondari za Serikali Kumb. Na. DC. 297/ 507/01/146 ya tarehe 23 Novemba, 2015;

v. Barua ya Katibu Mkuu TAMISEMI Kumb. Na. DC.297/507/01/145 ya tarehe 27 Novemba, 2015 kuhusu Ugharimiaji wa Elimu ya Awali na Elimumsingi bila malipo Tanzania Bara kuanzia Januari 2016;

vi. Barua ya Katibu Mkuu TAMISEMI ya tarehe 23/11/2015 kuhusu Utaratibu wa Uandikishaji wa Darasa la Kwanza Mwaka 2016;

## 2.0. Maana ya Elimumsingi bila malipo

Utoaji wa Elimumsingi bila malipo una maana ya kwamba mwanafunzi atasoma bila mzazi/mlezi kulipa ada wala michango ya fedha iliyokuwa ikitozwa shuleni kabla ya kutolewa kwa Waraka wa Elimu namba 5 wa mwaka 2015.

Serikali itagharimia ada ya mwanafunzi wa shule ya sekondari ya kutwa na bweni iliyokuwa inatolewa na mzazi au mlezi kwa shule za Serikali. Kabla ya Waraka huu kutolewa, wazazi/walezi walikuwa wanalipa ada na michango mbalimbali kama ilivyoidhinishwa kwenye nyaraka zifuatazo:

i. Waraka wa Elimu Namba 9 wa mwaka 1998 ulioelekeza tozo la ada ya shilingi 40,000/= kwa mwanafunzi wa shule ya kutwa na 70,000/= kwa mwanafunzi wa bweni;

ii. Waraka wa Elimu Namba 11 wa mwaka 2004 uliopunguza ada kwa wanafunzi wa kutwa kutoka shilingi 40,000/= hadi 20,000/= kwa kila mwanafunzi;

iii. Waraka wa Elimu Namba 8 wa Mwaka 2011 kuhusu michango mbalimbali wanayotakiwa kutoa wazazi/walezi kulingana na makubaliano yao kupitia Kamati/Bodi za shule;

iv. Waraka wa Elimu Namba 1 wa mwaka 2012 kuhusu kurejesha ada ya mtihani kwa shule Sekondari za Serikali; na

v. Waraka wa Elimu Namba 1 wa mwaka 2013 wa kuchangia gharama za Ukaguzi wa Shule kwa kiwango cha jumla ya shilingi 1,000/= kwa kila mwanafunzi wa shule za Sekondari zisizo za Serikali.

Aidha, fomu za kujiunga na Shule nazo zilitoa maelekezo mbalimbali kuhusu malipo yanayotakiwa kufanyika kabla mwanafunzi hajapokelewa shuleni.

Kufuatia Waraka wa Elimu Namba 5 wa mwaka 2015 na utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 kuhusu utoaji wa Elimumsingi bila malipo, Serikali sasa imefuta nyaraka zote kuhusu malipo yaliyokuwa yakitozwa katika uendeshaji wa Elimumsingi kutoka kwa wazazi/walezi kwenye Shule za Serikali. Waraka wa Elimu Namba 1 wa mwaka 2013 wa kuchangia gharama za Ukaguzi wa Shule utaendelea kutumika.

## 3.0. Majukumu katika utaratibu wa Elimumsingi bila malipo

Katika kutekeleza Elimumsingi bila malipo, majukumu ya Serikali, wazazi/walezi, Wakuu wa Shule na Kamati/Bodi za Shule na jamii kwa ujumla kuhusu utekelezaji wa elimu bila malipo yatakuwa kama ifuatavyo:

### 3.1. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WEST)

Jukumu la **Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia** ni kufanya yafuatayo:

i. Kutoa nyaraka za mambo ya kuzingatiwa katika utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 katika utoaji wa Elimumsingi bila malipo;

ii. Kutenga fedha za kugharimia utayarishaji wa mitihani ya kitaifa kulingana na idadi ya wanafunzi walio katika shule za Serikali;

iii. Kutenga fedha kwa ajili Uthibiti Ubora wa Shule; na

iv. Kutenga fedha za kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utoaji wa Elimumsingi bila malipo na kuchukua hatua stahiki pale inapobidi.

### 3.2. Ofisi ya Rais - TAMISEMI:

i. kutafsiri na kusimamia utekelezaji wa Elimumsingi bila malipo kulingana na nyaraka, miongozo na maelekezo kadri inavyotolewa na WEST;

ii. kutoa miongozo mbalimbali kwa Wakuu wa Shule juu ya uandikishaji wa watoto wa Elimu ya Awali, Darasa la Kwanza na Kidato cha Nne;
iii. kutoa miongozo ya matumizi ya fedha za umma kwa Wakuu wa Shule;
iv. kuratibu uandaaji wa mipango na bajeti ili kupata mipango na bajeti ya taifa kila mwaka inayozingatia mahitaji halisi ya Elimumsingi bila malipo;
v. kufanya ukaguzi wa ndani, ufuatiliaji na tathmini za mara kwa mara ili kuhakikisha Elimumsingi bila malipo inatolewa kwa ufanisi na viwango vya ubora vinavyostahili; na
vi. kutoa taarifa mbalimbali kwa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia zitakazosaidia katika kuandaa taarifa za jumla za sekta ya elimu na mafunzo au kutoa maamuzi kuhusu masuala yanayojitokeza wakati wa utekelezaji.
vii. kutenga fedha za Ruzuku ya Uendeshaji wa Shule (Capitation Grant);asilimia 50% elimu ya sekondari na asilimia 40% elimu ya msingi kwa ajili ya kununua vitabu.

### 3.3. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa:

i. kupokea, kutafsiri na kusambaza nyaraka na miongozo kuhusu utoaji wa elimu bila malipo;

ii. kupokea maombi na kutoa kibali cha wazazi/walezi kuchangia huduma ya chakula cha mchana kwa wanafunzi wa kutwa na Chakula na huduma nyingine kwa wanafunzi wa Hosteli;
iii. kuratibu mapendekezo ya mipango ya bajeti za Halmashauri na mahitaji halisi ya elimu bila malipo;
iv. kufuatilia na kushauri kuhusu taratibu za utoaji wa Elimu bila malipo;
v. kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria kwa wanaokiuka taratibu za elimu bila malipo.

### 3.4 Ofisi ya Mkuu wa Wilaya:

i. kuchukua hatua za kinidhamu na kisheria kwa wanaokiuka taratibu za elimu bila malipo ndani ya wilaya;
ii. kufuatilia utekelezaji wa elimu bila malipo;

iii. kuwachukulia hatua wazazi/walezi wanaoshindwa kuwaandikisha watoto shule na kusimamia mahudhurio na maendeleo ya taaluma yao.
iv. kutenga fedha za kuratibu uendeshaji na usimamizi wa mitihani ya kitaifa

## 3.5. Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji:

i. kuandaa mipango na bajeti kila mwaka inayozingatia mahitaji halisi ya Elimumsingi bila malipo, bila kusahau mahitaji ya wanafunzi na walimu, na kusimamia utekelezaji wake kwa ufanisi. Mipango na bajeti hizi zihusishe pia watoto wote wenye umri wa rika lengwa waliopo katika vituo shikizi, na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi katika ngazi hiyo;
ii. kuratibu utoaji mipango na bajeti za ruzuku ya uendeshaji wa Shule ikiwemo ulinzi, umeme, maji na ununuzi wa chaki na karatasi pamoja na vifaa vingine vya kufundishia na kujifunzia;
iii. kuandaa Takwimu sahihi za wanafunzi wote zikiainisha wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa kila shule vikiwemo vitengo na shule zisizo za Serikali;
iv. kutenga na kutuma fedha shuleni kwa wakati kwa ajili ya uendeshaji na usimamizi wa mitihani na majaribio mbalimbali shuleni ikiwemo tathmini endelezi;
v. kutenga fedha ya Ruzuku ya Uendeshaji wa Shule; asilimia 60% elimu ya msingi na asilimia 50%elimu ya sekondari kwa ajili ya kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wa elimu maalum;
v. kutenga na kutuma fedha shuleni za kununua samani yakiwemo madawati, vifaa vya michezo, matengenezo ya mashine na mitambo pamoja na kujenga na kukarabati miundombinu ya Shule;
vi. kutenga na kutuma fedha shuleni za kugharimia chakula wanafunzi wa kutwa na wa bweni, nauli wakati wa kwenda na kurudi likizo pamoja na vifaa na visaidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum waliopo kwenye Shule na Vitengo vya Elimu Maalum;
vii. kutenga na kutuma fedha shuleni za usimamizi na utoaji wa elimu ya watu wazima kwa kugharimia vifaa vya

wanafunzi katika kutekeleza nyaraka mbalimbali za Elimumsingi bila malipo;

vi. kushirikiana na jamii kuweka utaratibu wa kutoa huduma ya chakula cha mchana kwa wanafunzi wa kutwa au kutoa chakula na huduma nyingine kwa wanafunzi wa Hosteli na kupeleka maombi kwa Katibu Tawala wa Mkoa kupitia kwa Mkurugenzi wa Halmashuri husika;

vii. kushirikiana na walimu katika kubainisha changamoto zitokanazo na mpango wa utekelezaji wa elimu bila malipo na kuwasilisha mapendekezo kwa Mkurugenzi wa halmashauri;

viii. kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia;

ix. kuandikisha watoto wote wenye umri wa kuanza shule bila masharti au malipo yoyote; na

x. kugawa, kwa wanafunzi waliofaulu, fomu ya kujiunga na shule iliyotolewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI.

### 3.7. Kamati/Bodi za Shule za Serikali

Kamati na Bodi za Shule za Serikali zitaendelea kuwa kiungo muhimu cha wazazi na walezi na Shule. Aidha zihakikishe kuwa zinasimamia vema uendeshaji wa Shule ikiwemo:

i. kufuatilia na kusimamia matumizi ya fedha zote za shule ili ziweze kuleta tija;
ii. kuhakikisha kuwa sera, nyaraka, maelekezo na miongozo ya Serikali inazingatiwa na kutoa ushauri stahiki;
iii. kuishirikisha jamii katika maazimio ya masuala mbalimbali yanayohusu maslahi na maendeleo ya Shule kwa ujumla kama vile ulinzi na upatikanaji wa walimu wa muda (temporary/part time teachers) kwa masomo ya Sayansi, Hisabati na Ufundi. Maazimio yanayohusu uchangiaji wa hiari, yawasilishwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kwa lengo la kupata Kibali;
iv. kushirikiana na wazazi/jamii kuweka utaratibu wa chakula cha mchana au chakula na huduma za Hosteli katika shule

kufundishia na kujifunzia pamoja na malipo ya honoraria kwa walimu wanaofundisha madarasa husika;

viii. kutenga na kutuma fedha shuleni kwa ajili ya watoto walioko kwenye mazingira hatarishi, yatima na wengine wa aina hiyo kulingana na miongozo ya Serikali kuhusu masuala haya;

ix. kusambaza miongozo ya Elimumsingi bila malipo na kukagua matumizi sahihi ya fedha na ruzuku za uendeshaji wa shule,

x. kuendelea kutoa elimu kwa umma na kuhamasisha jamii katika kujitolea nguvukazi na mali ili kuleta ustawi na maendeleo ya Shule zilizoko ndani ya jamii husika;

xi. kutathmini Mazingira ya shule za kutwa na kumshauri Katibu Tawala Mkoa kuhusu kutoa kibali cha huduma za chakula cha mchana au chakula na huduma kwa wanafunzi wa Hosteli;

xii. kutenga fedha za kugharimia uendeshaji wa mitihani ya kitaifa kulingana na idadi ya wanafunzi walio katika shule za Serikali;

xiii. kuweka mipango na bajeti kwa ajili ya kutoa motisha kwa walimu na wanafunzi wanaofanya vizuri katika masomo, vipaji na vipawa.

### 3.6. Wakuu wa Shule za Serikali

Wakuu wa Shule watafanya yafuatayo:

i. kusimamia shughuli zote za taaluma, utawala na uendeshaji wa Shule;

ii. kuwapa maelekezo wazazi kuhusu aina ya vifaa vinavyohitajika mfano rangi ya kitambaa cha sare ya Shule, sare za michezo, idadi na aina ya madaftari watakayotumia wanafunzi ili wazazi waweze kununua wenyewe;

iii. kusimamia na kuhakikisha kwamba fedha inayotolewa na Serikali inatumika kama ilivyokusudiwa kulingana na taratibu za fedha za Serikali;

iv. kutoa takwimu na taarifa sahihi za idadi ya wanafunzi na mahitaji mengine ya Shule;

v. kuanzisha jukwaa la wazazi na walimu ili kujadiliana masuala mbalimbali kuhusu maendeleao ya Shule na

za kutwa kulingana na mazingira yao, na kutuma mapendekezo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri.

### 3.8. Walimu

Walimu wana nafasi kubwa katika kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu bora kulingana na mazingira yaliyopo. Kila Mwalimu ahakikishe kuwa:

i. anazingatia sera, nyaraka, maelekezo na miongozo ya Serikali kuhusu utoaji Elimumsingi bila malipo;

ii. anatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa kazi yake ikiwemo kutoa mrejesho kwa mzazi/mlezi kuhusiana na maendeleo ya mtoto wake;

iii. anawaongoza na kuwasaidia wanafunzi kupata elimu bora na kukua katika maadili mema ili waweze kuwa raia wema watakaoshiriki kikamilifu katika maendeleo yao, familia, jamii na taifa kwa ujumla;

iv. anakuwa na maadili mema na utendaji uliotukuka siku zote ili awe mfano wa kuigwa na wanafunzi wake; na

v. anatoa ushauri nasaha na unasihi kwa watoto wenye matatizo mbalimbali ya kijamii na kitaaluma.

### 3.9. Wanafunzi

Wanafunzi ambao ndiyo walengwa wa Elimumsingi bila malipo wana majukumu yafuatayo:

i. kwenda Shule na kuhudhuria masomo kulingana na ratiba ya Shule;

ii. kuwa na maadili mema wakati wote na hivyo kuacha kujihusisha na vitendo vya uvunjaji wa kanuni mbalimbali za Shule na Sheria za Nchi;

iii. kutoa mrejesho kwa wazazi/walezi kuhusu alichojifunza ili wafahamu na kuweza kumsaidia ipasavyo katika masomo yake;

iv. kutoa mrejesho kwa wazazi/walezi kuhusu jambo lolote linaloagizwa shuleni ili mzazi/mlezi ashiriki kikamilifu katika maendeleo ya shule.

## 3.10. Wazazi/Walezi

Wazazi/walezi watakuwa na majukumu yafuatayo:

i. kununua sare za Shule na michezo, vifaa vya kujifunzia vikiwemo madaftari na kalamu pamoja na kugharimia matibabu kwa watoto wao;

ii. kununua magodoro, shuka, vifaa vya usafi binafsi kwa wanafunzi wanaosoma Shule za bweni na wanaoishi katika Hosteli zinazotumiwa na serikali;

iii. kushirikiana na uongozi wa shule kuweka utaratibu wa kutoa chakula cha mchana kwa shule za kutwa na zenye Hosteli kulingana na mazingira yao. Makubaliano yawasilishwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kwa ajili ya kibali.

iv. kulipia nauli ya kwenda Shule na kurudi kwa wanafunzi wa kutwa, hosteli na wa bweni wakati wa likizo;

v. kukemea na kutoa taarifa kwa ngazi husika kuhusu mienendo inayokwenda kinyume na Elimumsingi bila malipo; na

vi. Kufuatilia mahudhurio na maendeleo ya taaluma ya watoto wao.

## 3.11. Viongozi na Jamii katika mamlaka za Vijiji na Mitaa

Shule ni sehemu ya jamii. Hivyo, viongozi na jamii zinazozunguka Shule zitaendelea kuwa na wajibu wa:

i. kuhamasisha wazazi/walezi wenye watoto wenye umri wa kwenda shule wanaandikishwa shuleni;

ii. kufuatilia na kutoa ushirikiano kwa shule na wazazi/walezi katika kuhakikisha kwamba wanafunzi wanakuwa shuleni wakati wa masomo badala ya kuzurura mitaani au kuwa kwenye shughuli ambazo hazihusiani na masomo;

iii. kutoa ushirikiano katika shughuli zote za kuleta maendeleo ya kielimu katika maeneo yao ili kuweza kupata matokeo tarajiwa kwa wakati; na

iv. kuendelea kujitolea nguvukazi na mali ili kuleta ustawi na maendeleo ya Shule zilizoko ndani ya jamii.

### 3.12. Angalizo

Waraka huu hauzihusu:

i. Shule za Serikali zifuatazo:
   a. Shule ya Msingi Arusha (Arusha);
   b. Shule ya Msingi Kisimani (Arusha)
   c. Shule ya Msingi Olympio (Dar es Salaam);
   d. Shule ya Msingi Diamond (Dar es Salaam);
   e. Shule ya Msingi Oysterbay (Dar es Salaam);
   f. Shule ya Msingi Iringa (Iringa);
   g. Shule ya Msingi Mkapa (Mbeya);
   h. Shule ya Msingi Angaza (Mbeya);
   i. Shule ya Msingi Nuru (Mbeya);
   j. Shule ya Msingi Lupilisi (Ruvuma); na
   k. Shule ya Msingi Changa (Tanga); na

ii. Shule zinazomilikiwa na mashirika ya umma ama taasisi za umma ambazo zinaendeshwa kwa taratibu sawa na Shule za binafsi.

Kwa sasa Shule hizi zitaendelea na utaratibu uliopo kuhusu Shule hizo hadi waraka mpya utakapotoka.

Waraka huu unafuta Waraka wa Elimu Namba 6 wa Mwaka 2015 na unaanza kutumika kuanzia tarehe 1/6/2016.

Prof. Eustella P. Bhalalusesa
**KAMISHNA WA ELIMU**